# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA MSAJILI WA HAZINA

Anwani ya simu: Msajili wa Hazina,
Dar es Salaam
Simu Nambari: 2121334/ Fax: 2110046
Barua pepe: tr@tro.go.tz
*(Mawasiliano yote ya kiofisi yaandikwe kwa Msajili wa Hazina na SIYO kwa mtu binafsi)*

Jengo la CHC,
33 Mtaa wa Samora/Mirambo 50,
Sanduku la Barua 3193,
**11104 DAR ES SALAAM.**

**Unapojibu tafadhali taja:**

**Kumb. Na. CCA.136/171/01/87** **24 Desemba, 2024**

Watendaji Mkuu,

Wakala, Taasisi na Mashirika ya Umma,

**TANZANIA BARA.**

**KUH: MWONGOZO WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/26 PAMOJA NA MAELEKEZO MAHSUSI KWA WAKALA, TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

2. Napenda kuwataarifu kuwa, mwongozo wa mpango na bajeti kwa mwaka 2025/26 umekamilika na unapatikana katika tovuti ya Wizara ya Fedha (www.mof.go.tz) na tovuti ya Ofisi ya Msajili wa Hazina (www.tro.go.tz).

3. Pamoja na mwongozo huo, tumeandaa maelekezo mahsusi kwa Taasisi na Mashirika ya umma ambayo yanazingatia tathmini ya zoezi la uchambuzi wa bajeti kwa mwaka 2024/25, na maeneo mengine ambayo hayakufafanuliwa kwa kina katika mwongozo. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo: -

### 3.1. Bajeti ya Mchango kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali

Taasisi na Mashirika yote yanatakiwa kutenga katika bajeti zao kiasi kinachopaswa kuwasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali kutoka katika mapato ya ndani kwa kutumia Geresho lilioainishwa katika Mwongozo wa Bajeti. Aidha, Mashirika yanayowasilisha asilimia 15% ya mapato ghafi katika Mfuko Mkuu wa Serikali, zinaelekezwa kuzingatia uwiano wa asilimia 85 kwa asilimia 15 katika kupanga matumizi ya kila mwezi ili kutoathiri kazi za Mashirika husika pamoja na uwasilishaji wa michango hiyo.

Mashirika ya kibiashara yanayotoa gawio yanatakiwa kuzingatia utaratibu wa kutoa gawio la awali (Interim dividend) na gawio la mwisho (Final dividend) kulingana na hali ya kifedha

ya Shirika husika. Aidha, Mashirika hayo yawasilishe makisio ya hesabu kwa mwaka 2025/26 (Projected Financials) kwa kuambatisha katika Mfumo wa PlanRep.

Mashirika yanayotoa mchango wa maendeleo yanahimizwa kuendelea kufanya hivyo kwa kuzingatia hali ya kifedha ya Taasisi au Shirika husika. Mashirika yote yanatakiwa kuandaa mtiririko wa fedha (Cash Flow), inayoonesha mwezi wa kuwasilisha michango hiyo na kuambatisha kwenye mfumo wa PlanRep.

### 3.2 Uandaaji na uchambuzi wa Bajeti ya mwaka 2025/26

Taasisi na Mashirika ya umma yanakumbushwa kuwa bajeti zote kwa mwaka 2025/26 zitaandaliwa na kufanyiwa uchambuzi kupitia mfumo wa Bajeti wa PlanRep pekee kwa ajili ya majumuisho katika Bajeti ya Serikali.

### 3.3 Mapitio ya Bajeti ya nusu mwaka 2024/25 (Mid-year review 2024/25)

Tunapenda kuwafahamisha kwamba mfumo unafunguliwa tarehe 01 Januari, 20245 kwa ajili ya mapitio ya nusu mwaka ya bajeti ya 2024/25. Taasisi na Mashirika ya umma yanatakiwa kufanya mapitio kwa kulinganisha makadirio na utekelezaji uliofanyika katika kipindi cha miezi 6 na uhamisho wa fedha kutoka kifungu kimoja kwenda kifungu kingine (reallocation within) kulingana na uhalisia wa utekelezaji wa bajeti. Zoezi hili linatekelezwa kuzingatia masharti yaliyowekwa kupitia Sheria ya Bajeti
Sura 439 na kanuni zake.

### 3.4 Matumizi ya geresho sahihi (GFS code)

Taasisi na Mashirika ya Umma yanakumbushwa matumizi ya geresho sahihi kama ilivyofanyiwa maboresho Disemba 2023. Hatua hii itasaidia kurahisisha uhamishaji wa vifungu vya bajeti kutoka kwenye mfumo wa PlanRep kwenda kwenye mifumo ya utekelazaji wa bajeti (MUSE, NeST, NPMIS, NAVISION).

### 3.5 Idhini ya Maoteo ya Bajeti

Taasisi na Mashirika ya umma yanaelekezwa kuwasilisha bajeti zake kwenye mfumo wa PlanRep zikiwa na idhini ya mwenyekiti wa Bodi na Mtendaji Mkuu. Kwa Taasisi ambazo hazina Mwenyeviti wa Bodi, Katibu Mkuu wa Wizara husika anaweza kutoa idhini hiyo kwa mujibu wa Sheria. Hivyo, Taasisi na Mashirika ya Umma yanaelekezwa kuhakikisha kuwa vikao vya Bodi na Mabaraza ya wafanyakazi vinafanyika Mwezi
Januari ili kuwezesha uwasilishwaji wa bajeti hizo.

### 3.6 Miradi ya Maendeleo

Taasisi na Mashirika ya Umma zinaelekezwa kusajili Miradi yote inayotegemea kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2025/26 katika mfumo wa miradi (NPMIS).

### 3.7 Idhini na Matumizi ya Fedha zilizovuka Mwaka (Carry Over Fund)

Mashirika na Taasisi za umma zinakumbushwa kuomba kibali cha fedha za kuvuka mwaka endapo kuna miradi iliyotengewa fedha katika mwaka 2024/25 na haitoweza kukamilika ndani ya mwaka husika kwa mujibu wa sheria na kanuni za bajeti.

### 3.8 Kuwasilisha taarifa za utendaji za kila robo mwaka na taarifa za mwaka

Taasisi na Mashirika ya umma yanakumbushwa kuwasilisha taarifa za utendaji za kila robo mwaka sambamba na taarifa za utekelezaji wa mikataba ya utendaji katika Ofisi ya Msajili wa Hazina kama ilivyoelekezwa katika mwongozo wa Bajeti.

### 3.9 Muda wa kuwasilisha Bajeti

Mfumo kwa ajili ya uandaaji wa Bajeti ya mwaka 2025/26 utafunguliwa rasmi tarehe 6 Januari 2025 na Bajeti zinatakiwa kuwasilishwa kabla ya tarehe 28 Februari 2025. Mwenyekiti na Mtendaji Mkuu wa Mashirika wanatakiwa kuzingatia muda wa uwasilishaji wa Bajeti za Mashirika yao.

### 3.10 Mikataba ya Utendaji kazi kati ya Msajili wa Hazina na Wenyeviti wa Bodi wa Taasisi na Mashirika ya umma

Msajili wa Hazina anatakiwa kuingia mikataba ya utendaji na wenyeviti wa Bodi wa Taasisi na Mashirika ya umma ikiwa ni utekelezaji wa kifungu cha 10(2) (k) cha Sheria ya Msajili wa Hazina Madaraka na Majukumu SURA 370. Ili kurahisisha utekelezaji wa kifungu hicho,

unatakiwa baada ya kukamilisha kuandaa mpango na bajeti wa mwaka 2025/26 kuandaa rasimu ya mkataba wa utendaji kati ya Msajili wa Hazina na Mwenyekiti wa Bodi kwa kuingiza malengo katika mkataba huo ili uweze kukamilishwa ifikapo tarehe 30 Juni, 2025 kabla ya kuanza mwaka mpya wa fedha 2025/26.

4. Tunashukuru kwa ushirikiano wenu,

Lightness Mauki

**Kny: MSAJILI WA HAZINA**